Umoja wa Nchi Huru za Africa

# HOTUBA YA
# DR. SALIM AHMED SALIM,
# KATIBU MKUU, UMOJA WA NCHI HURU ZA AFRIKA,
# KATIKA UZINDUZI WA JUMUIYA YA AFRIKA MASHARIKI

**ARUSHA, TANZANIA**

**15 JANUARI 2001**

**Mheshimiwa Rais Daniel arap Moi, Rais wa Jamhuri ya Kenya,**

**Mheshimiwa Rais Yoweri Kaguta Museveni, Rais wa Jamhuri ya Uganda,**

**Mheshimiwa Rais Benjamin William Mkapa, Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania,**

**Mheshimiwa Rais Pierre Buyoya, Rais wa Jamhuri ya Burundi,**

**Mheshimiwa Rais Paul Kagame, Rais wa Jamhuri ya Rwanda,**

**Mheshimiwa Dr. Omar Ali Juma, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,**

**Mheshimiwa Amani Abed Karume, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi,**

**Mheshimiwa Frederick Sumaye, Waziri Mkuu wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania**

**Waheshimiwa Mawaziri,**

**Waheshimiwa mabalozi na wawakilishi walioalikwa,**

**Mheshimiwa Katibu Mkuu wa Jumuia ya Afrika ya Mashariki,**

**Mabibi na Mabwana,**

Leo ni siku adhimu kwa wananchi wa Afrika ya Mashariki. Pia ni siku ya kihistoria kwa Waafrika wote popote pale walipo katika bara letu.

Kwa wananchi na viongozi wa Afrika ya Mashariki, kuasisiwa upya kwa Jumuia ambayo itadumisha na kuimarisha ushirikiano na mshikamano ni hatua kubwa katika uhai wa mataifa matatu haya ya eneo hili la bara letu. Tukio hili la kusheherekewa na kujivunia linatoa matumaini makubwa katika maisha ya watu wetu katika nyanja mbali mbali. Hususan, uwezo wa nchi zetu hizi tatu wa kupeleka mbele gurudumu la maendeleo na kupiga vita umasikini na unyonge utaongezeka kwa kiwango kikubwa. Ushirikiano huu pia utaimarisha uelewano, utulivu na amani katika Afrika ya Mashariki.

Kutokana na hatua hii ni dhahiri kwamba MAFANIKIO HAYA NI MAFANIKIO YA AFRIKA NZIMA. Ni ukweli usiotetereka kwamba tukio lolote lile linaloathiri vibaya nchi au mkusanyiko wa nchi katika sehemu yeyote ya bara letu basi huathiri vibaya bara lote. Kwa mfano, majanga

yanayosababishwa na binadamu kama vile vita vya wenyewe kwa wenyewe, au ukiukaji wa haki za binadamu au kukandamizwa kwa demokrasia yatokeyapo katika sehemu yeyote ya bara letu hupaka matope bara zima. Kwa mantiki hiyo hiyo hatua za maendeleo na kuleta mshikamano kama hii tunayoisheherekea hapa Arusha leo sio tuu ni changamoto ya maana kwetu sote na kuimarisha nguvu zetu, bali pia inalipatia bara letu heshima duniani. Kusema kweli, sura ya bara letu mbele ya watu wetu na jamii ya kimataifa itakuwa ya kuridhisha sana kwa matukio kama haya badala ya kuwa na mtiririko wa misukosuko kila leo na hasa ile ya kujitakia.

Kwa hiyo basi, napenda kuchukua nafasi hii kutoa pongezi za dhati kwa niaba ya Umoja wa Nchi Huru za Afrika na kwa niaba yangu mwenyewe kwa viongozi na wananchi wote wa Afrika ya Mashariki kwa tukio hili adhimu na la kihistoria.

**Waheshimiwa Viongozi na Ndugu Wananchi,**

Ni dhahiri kwamba hivi sasa Afrika imejizatiti kujenga mshikamano na kuifikia nia ya muda mrefu ya kuwa umoja imara zaidi wa Nchi zetu zote. Katika dhamiri hiyo, kila hatua tunayopiga ya baadhi ya nchi kuimarisha ushirikiano wao, basi unachangia katika kufanikisha lengo letu hilo tukufu kwa bara letu. Kwa hiyo, naomba nirejee kusema kwamba siku ya leo ina umuhimu kwa Waafrika wote.

Tumeingia katika karne ya 21 na pia katika milenia mpya katika namna ambayo bara letu linakabiliwa na hali ya dunia inayohitaji ushirikiano na mshikamano baina ya nchi na miongoni mwa jamii. Hatutaweza asilan kuyamudu matatizo yaliopo au hata kufaidika na maendeleo ya teknolojia na mawasiliano ikiwa tutabaki katika uhusiano wa kutengana. Kama walivyotuusia viongozi waasisi wa Afrika huru– Umoja siku zote ndio Nguvu Yetu na ndio Mtaji wetu.

Nyenzo madhubuti katika harakati za kupambana na umasikini uliozagaa katika nchi zetu na katika kuleta maendeleo ya haraka ni ushirikiano na mshikamano. Kwa kweli, hata sababu zinazoleta wgomvi na vita vya mara kwa mara vinavyotokea miongoni mwetu tunaweza kuziondoa kwa kudumisha umoja na ushirikiano. Aidha, hata masahibu kama balaa la ukimwi, na majanga ya ukame, mafuriko, na ajali nyingi zinazotokea tunaweza kukabiliana nazo kwa nguvu zaidi ikiwa tuna umoja.

Wananchi wa Afrika Mashariki wanayo bahati ya kihistoria, kijamii, na hata kijiografia. Ipo historia ndefu ya kiwango cha juu cha ushirikiano katika eneo hili. Hadi inavunjika Jumuia ya Afrika ya Mashariki mwaka 1977, nchi hizi tatu zilikuwa na kiwango cha

ushirikiano katika maeneo kadhaa kupita hata jumuia ya Ulaya. Uzoefu uliopatikana wakati ule na hata athari zilizojitokeza ilipovunjwa Jumuia zinatoa mafunzo mengi yatakayosaidia kuimarisha ushirikiano unaorejeshwa.

Vile vile, uhusiano uliojengeka baina ya watu wa nchi hizi tatu na kukaribiana kwao katika mila na utamaduni, kwa kutumia lugha ya kiswahili, na maelewano yao ya siku nyingi, ni mambo yanayoweka msingi madhubuti wa kudumisha ushirikiano. Pamoja na hilo, nchi hizi zimejaaliwa pia na muundo wa kijiografia. Kila moja imepakana na nyingine mbili na hivyo kuwezesha zote tatu kuwa na ujirani wa karibu sana kwa pamoja. Hali hii, kwa kiasi fulani inasaidia mawasiliano na pia imeimarisha uhusiano wa kijamii. Hivyo basi, haieleweki kwa nchi hizi kutafuta maendeleo yake kwa kutengana.

Tunaamini kwamba kuimarika kwa Ushirikiano wa nchi hizi tatu kunaongeza nguvu za jumuia nyingine katika bara letu, kama vile SADC inayojumuisha nchi za kusini, COMESA inayojumuisha nchi za Mashariki, kusini, kaskazini na kati ya Afrika, ECOWAS ya Afrika magharibi, ECCAS ya Afrika ya kati, UMA ya Afrika kaskazini, IGAD ya nchi za pembe ya Afrika, na pia CEN-SAD inayoshirikisha nchi kadhaa kutoka maeneo mbali mbali ya bara letu.

Malengo muhimu ya Jumuia hizi ni kukuza, kuimarisha, na kupanua ushirikiano na mshikamano wa nchi zinazohusika. Lakini pia tusisahau dira yetu kubwa zaidi ya pamoja. Nayo ni kuandaa mazingira ambayo yatahakikisha kufanikiwa kuleta umoja, ushirikiano kamambe na kuasisiwa kwa Jumuia ya Ushirikiano ya Afrika nzima na kuleta umoja wa bara zima. Lakini ni vizuri kusisitiza kwamba lengo hilo litapatikana kwa kuimarisha na kutanua mafanikio kama haya ya leo.

Kutokana na uzoefu tulioupata kutokana na ushirikiano wa siku za nyuma inaridhisha kuona kwamba viongozi wa Afrika Mashariki wamechukua muda kutafakari kwa kina kuasisiwa upya kwa ushirikiano ili kuepuka makosa yaliopita na kuhakikisha kwamba Jumuia mpya na taasisi zake zinajengwa katika msingi imara. Aidha, inatia moyo kuona kwamba Jumuia hii inaanzishwa kwa kutoa nafasi kubwa sana kwa mshikamano wa wananchi wenyewe wa Afrika Mashariki katika nyanja tofauti. Kwa kudumisha ushirikiano katika sekta binafsi, sekta ya kijamii, na sekta ya serikali na umma, Jumuia itaimarisha mizizi madhubuti miongoni mwa wananchi wenyewe.

Ni wazi kwamba tumefika hapa tulipofika leo kutokana na ujasiri na hekima ya viongozi wetu wa Afrika ya Mashariki wakiungwa mkono na wananchi katika kufikia siku hii ya leo.

Tunawapongeza kwa dhati kabisa kwa mafanikio haya na tuna imani kwamba wataendelea katika msimamo huu thabiti. Pia ni wazi

kwamba juhudi za watu wengi na sekta mbali mbali zimechangia. Ningependa kutambua juhudi maalum za Baraza la Mawaziri wa nchi tatu hizi kwa kazi nzuri waliofanya na pia kutambua kazi iliyofanywa na Katibu Mkuu wa Jumuia, Balozi Francis Muthaura na wasaidizi wake na pia sekretariati yote ya Jumuia.

Umoja wa Nchi Huru za Afrika itashirikiana bega kwa bega na viongozi na wananchi wa Afrika Mashariki katika kudumisha ushirikiano na mshikamano katika Afrika Mashariki na katika bara letu kwa ujumla.

Asanteni sana.